JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

Namba za simu;

Mkuu wa Shule: +255 784 369 381

Makamu Mkuu wa Shule: +255 787 448 383

Matron / Patron ……

Shule ya Sekondari **MIONO**

S.L.P 26 - CHALINZE

Tarehe 23.5.2018

Mzazi /Mlezi wa Mwanafunzi ……..

……..

S.L.P …….

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI

MIONO HALMASHAURI YA _CHALINZE_ MKOA WA Pwani MWAKA 2018/2019

1. Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2018/2019 tahasusi ya ……. Shule ya Sekondari MIONO ipo katika kijiji cha Makao Makuu, Kata ya **MIONO**, Tarafa ya Miono.kijiji hiki kipo karibu na eneo la MTO WAMI katika barabara kuu ya **CHALINZE-SEGERA**, ukitokea Chalinze shuka MANDERA (baaada ya kuvuka daraja la MTO WAMI) ambapo ni njia panda ya kuelekea MIONO, utakwenda mwendo wa kilometa 20 kutokea MANDERA hadi kufika shuleni.Aidha ukitokea **SEGERA** shuka kituo cha MANDERA kabla ya WAMI.Kwa wanaotokea Dar es salaam nenda kituo cha mabasi cha Mbezi, panda mabasi ya DAR-MIONO au DAR- SAADANI ambayo yanafika MIONO. Nauli ni shilingi elfu saba (7000/=) kutokea Mbezi, na shilingi elfu nne kutokea Chalinze.nauli ya boda boda kutoka MIONO hadi shuleni ni shs.2,500/=ukipanda gari inayoelekea Saadani utashushwa shuleni.usishuke Miono.

   Muhula wa masomo unaaza tarehe 2.**7.2018.**Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 2.7.2018. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 16.7.2018 akiwa na fomu zote zilizoambatanishwa katika maelekezo ya kujiunga, ziwe zimejazwa kikamilifu na wahusika na kuzikabidhi shuleni wakati wa usajili.

2.0 Sare ya Shule

2.1. WAVULANA:

I. Suruali 2 za heshima rangi ya dark blue zenye marinda mawili

II. Shati 2 za heshima rangi nyeupe **mikono mirefu,**

III. Viatu vya ngozi rangi nyeusi **SIO BUTI** vya kamba na visiwe na kisigino kirefu.

IV. Nguo za kufanyia kazi (shamba dress), Suruali mbili rangi ya light blue na fulana (T-shirt) mbili rangi ya deep blue, **zisiwe na collar wala maandishi.**

V. Soksi jozi mbili rangi nyeusi,

VI. Mkanda mweusi wa kawaida usio na urembo.

VII. Tai rangi ya dark blue.inayofanana na rangi ya suruali

VIII. T-shirt ya rangi ya kijivu (grey) yenye nembo ya shule inapatikana hapa shuleni.

IX. Shuka mbili rangi ya bluu bahari (*light blue)* na mto wenye foronya ya bluu bahari (light blue)

X. Sweta yenye rangi ya dark blue

Xi. Track suit rangi ya kijivu, raba na nguo za michezo (zingatia: nguo za michezo zimepangwa kwa tahasusi kama ifuatavyo, PCM rangi Nyekundu kama ya jezi ya simba, PCB rangi ya njano kama jezi ya yanga, CBG zambarau kama jezi ya Mbeya city.)

NB : uje na chandarua kwaajili ya kujikinga na mbu.

2.2 WASICHANA:

I. Sketi 2 za heshima rangi ya dark blue ndefu kuvuka magoti zenye marinda (rinda box mbele na nyuma na marinda mawili upande wa kulia na kushoto). Kitambaa kiwe kizito

II. Sketi moja ya heshima rangi ya bluu bahari (light blue) kwaajili ya kuvaa siku ya kwenda Msikitini au Kanisani.

III. Blauzi 2 za heshima rangi nyeupe**, mikono mirefu**,waislamu wanaruhusiwa kuvaa hijab

IV. Viatu vya ngozi rangi nyeusi **SIO BUTI** vyenye kamba na visiwe na kisigino kirefu,

V. Soksi rangi nyeupe

VI. Tai ya rangi ya dark blue.inayofanana na rangi ya sketi

VII. Kanga/kitenge doti 2

VIII. T-shirt ya rangi ya kijivu (grey) yenye nembo ya shule inapatikana hapa shuleni.

VIII. Magauni mawili ya heshima ya kushindia rangi ya pinki (1) na light blue (1) yawe ya marinda ya pasi (shamba dress) **kitambaa kizito**. T-shirt mbili rangi ya deep blue, **zisiwe na collar wala maandishi**

IX. Shuka mbili rangi ya pink na mto wenye foronya ya pink.

X. Sweta rangi ya dark blue.

Xi. Track suit rangi ya kijivu, raba na nguo za michezo (zingatia: nguo za michezo zimepangwa kwa tahasusi kama ifuatavyo, PCM rangi Nyekundu kama ya jezi ya simba, PCB rangi ya njano kama jezi ya yanga, CBG zambarau kama jezi ya Mbeya city.)

NB: uje na chandarua kwaajili ya kujikinga na Mbu.

3. Ada na Michango ya shule

a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000.00 kwa mwanafunzi wa bweni. Unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35,000.00 kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja

b) **Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-**

i. Shilingi 5,000/= kwaajli ya ukarabati wa samani.
ii. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha
iii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma
iv. Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi, na vibarua wengine
v. Shilingi 2,000/= nembo ya shule
vi. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza Tshs 5,000/= na Bima ya Afya 5,000/= (Wanafunzi washauriwe kujiunga na mfuko wa Bima ya Afya CHF kikaya)
vii. Tshirt yenye nembo ya shule shilingi 10,000/=
viii. Umeme 15,000/=
ix. Maji 15,000/=
x. Fedha ya tahadhari 5000/= (haitarejeshwa)

Angalizo: Jumla ya ada na michango kwa mwaka ni shilingi **188,000.00**

Fedha hizo zilipiwe kwenye Akaunti ya shule Namba **21110001592 MIONO SECONDARY SCHOOL FUND** katika Benki ya NMB (tafadhali andika jina la Mwanafunzi kwenye pay in slip)

Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

(i) Ream ya karatasi 1 (kwa mwaka)

(ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
(iii) Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia

(iv) Scientific calculator

(v) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe) visiwe plastiki

(vi) Ndoo mbili za kuhifadhia maji ndogo zenye mifuniko

picha 2 pasport size za mwanafunzi na Picha nne (4) za Wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.**ANGALIZO:** Mwanafunzi wa tahasusi ya **PCM** alete panga, wa tahasusi ya **PCB** alete jembe, wa tahasusi ya **CBG** alete fagio 2 (laini na gumu anayosoma).

4. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

(i) Wizi
(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa / utoro
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu,/ walezi na jamii kwa ujumla
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyeote yule.
(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usikubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
(vii) Kufuga ndevu
(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa ya kulevya
(ix) Uvutaji wa sigara.
(x) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa
(xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba
(xii) Kushiliki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sharia za nchi;
(xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
(xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
(xv) **Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule**
(xvi) Kudharau bendera ya Taifa
(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
(xviii) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

UTHIBITISHO WA KUKUBALI NAFASI YA KUINGIA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MIONO

SEHEMU A (ijazwe na mwanafunzi)

Mimi (jina kamili).....

Nilizaliwa tarehe..... mwezi..... mwaka .....

Mahali nilipozaliwa kijiji/Mtaa..... Wilaya.....

Mkoa..... Dini.....

Nakubali nafasi niliyopewa ya kuingia kidato cha TANO shule ya sekondari MIONO. Nathibitisha kuwa **nitatii na kuzifuata sheria na kanuni za shule** ambazo mwanafunzi analazimika kutekeleza nakutimiza. Najua na kuamini kuwa migomo na vurugu siyo njia sahihi ya kutatua matatizo katika jamii, hivyo **naahidi** kutoshiriki katika migomo wala vurugu zozote bali nitakuwa mstari wa mbele kutoa taarifa kwa uongozi wa shule ili uweze kutatua au kutafutia utatuzi wa changamoto zozote zitakazo jitokeza shuleni.

Saini..... tarehe.....

SEHEMU B (Ijazwe na mzazi/mlezi)

Mimi (jina kamili) .....

Wa kijiji cha/Mtaa wa.....Wilaya ya.....Mkoa wa.....

Kazi yangu ni..... Dini.....

Nambari ya simu.....

Nafurahi kupokea nafasi aliyopata mtoto wangu, nitatekeleza na kutimiza mahitaji yote ya mtoto wangu kulingana na maagizo ya shule. Pia **nitahakikisha mtoto anaenda shule kwa muda uliopangwa** na nitakuwa tayari wakati wowote kusaidiana na shule kumlea mtoto huyu kinidhamu
na kimaadili.

Saini ya mzazi/mlezi.....

Jina la mtendaji wa kijiji/Kata.....

Saini.....

Mwisho, Karibu sana Shule ya Sekondari MIONO ili ufaidike kwa kupata ELIMU BORA.

.....
ALLY A. MUYANGO
MKUU WA SHULE

FORM B (PART A)

PRESIDENTS' OFFICE

LOCAL GOVERNMENT AND REGIONAL ADMINISTRATION

MIONO HIGH SCHOOL
P.O.BOX 26
CHALINZE

TEL: +255 784 369 381 / +255 787 448 383

REF.NO:MSS/F.V.SEL/2018/2019/01

TO: THE MEDICAL OFFICER,

.....
RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION TO:

Mr. / MISS..... FORM 5 – 2017/2018

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for full time Schooling course. The Examination should include the following categories [i-iii].

Each category or sub-category of which will render the applicant ineligible in case of a Defect. Pregnancy [category IV] will also render a girl candidate ineligible to the course.

(i) (a) Eye

(b) Hearing

(c) Limbs

(d) Speech

(e) Venereal disease (s)

(f) Leprosy

(g) Epilepsy

(ii). Neuroses

(iii) Other serious diseases

(iv) Pregnancy

.....

ALLY A. MUYANGO

HEADMASTER

.....

Name, signature & official stamp

MEDICAL OFFIER INCHARGE